TANGAZO LA SERIKALI NA. 208 la tarehe 15/3/2019

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA
SURA 290

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 6(1) na (16(1)*

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MASOKO, MINADA NA MAGULIO) ZA HALMASHAURI YA JIJI LA TANGA, 2019

Jina la Sheria na mwanzo wa kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Ushuru wa Masoko, Minada na Magulio) za Halmashauri ya Jiji la Tanga za mwaka, 2019 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Jiji la Tanga.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa kama itaelekezwa vinginevyo.

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Jiji la Tanga.

"Kibanda" maana yake ni chumba au jengo lolote lililojengwa katika eneo la Soko au eneo lolote lililoruhusiwa na Halmashauri lijengwe kwa madhumuni ya kufanyia biashara.

"Kizimba" maana yake ni meza, nafasi, sehemu nyingine katika soko inayotumika kwa ajili ya kuuzia bidhaa katika eneo la soko la Halmashauri.

"Kodi ya pango" maana yake ni kiasi cha fedha ambacho kitatozwa na Halmashauri ikiwa ni malipo ya pango, kibanda, meza au vizimba vilivyomo katika masoko, magulio au maeneo yoyote ya Halmashauri kwa kipindi maalum.

"Masoko" maana yake ni maeneo yote yaliyotengwa na

Halmashauri kwa matumizi ya kuuza na kununua bidhaa mbalimbali.

"Mkuu wa Masoko" maana yake ni mtumishi yeyote ambaye ameteuliwa na Halmashauri kusimamia shughuli za masoko.

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Tanga au Afisa ye yote wa umma atakayeteuliwa kukaimu majukumu ya Mkurugenzi.

"Mkusanya Ushuru" maana yake ni mtumishi yeyote au wakala anayefanya kazi ya kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri.

"Ushuru" maana yake ni kiasi cha fedha ambacho kimepangwa na kutozwa na Halmashauri chini ya Sheria hii.

"Wakala wa Mapato" maana yake ni mtu yeyote, taasisi au kikundi cha watu ambao huteuliwa na Halmashauri kukusanya mapato katika Soko au gulio lolote la Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hizi.

"Kibali" maana yake ni idhini itakayotolewa na Mkuu wa Masoko kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

"Mfanyabiashara" maana yake ni mtu yeyote anayeuza bidhaa kwa jumla au rejareja kwenye soko au gulio ambalo limeruhusiwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Uanzishwaji wa masoko

4. Masoko yote kabla ya kuanzishwa kwake ndani ya Halmashauri yatatakiwa kupata kibali kutoka Halmashauri.

Muda wa Masoko Kuwa wazi

5.-(1) Masoko yote yatafunguliwa kwa shughuli za biashara kuanzia saa kumi na mbili asubuhi (12.00) hadi saa kumi na mbili jioni (12.00) muda huo unaweza kuongezwa baada ya kibali kutolewa na Halmashauri.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu cha 5(1), Kamati ya soko kwa kushirikiana na Mkuu wa Soko inaweza kufunga soko kwa ajili ya matengenezo au shughuli yoyote ile pale itakapo hitajika baada ya kutoa matangazo katika Soko husika.

Mamlaka na majukumu

6.-(1) Kutakuwa na Mkuu wa Soko ambaye atateuliwa na Halmashauri kutoka miongoni mwa watumishi wa

ya Mkuu wa Soko

Halmashauri ambaye atakuwa na mamlaka na majukumu yafuatayo;

(a) atakuwa Mkuu wa Soko.
(b) atakuwa na mamlaka ya kutoa maelekezo au utaratibu unaopaswa kutumiwa au kufuatwa ndani ya Soko.
(c) atakuwa ndiye msimamizi Mkuu wa Sheria Ndogo hizi ndani ya eneo la Soko.
(d) kusimamia utekelezaji wa shughuli za soko.
(e) kusimamia shughuli zote za mawakala wanao kusanya mapato chini ya mikataba ndani ya soko.
(f) kusimamia shughuli zote za mawakala wanaofanya usafi wa mazingira na uzoaji taka unaofanywa chini ya mikataba ndani ya soko.
(g) atakuwa mwakilishi wa Halmashauri katika mikutano ya wafanya biashara na wadau wa soko.
(h) atatekeleza majukumu mengine yoyote atakayo elekezwa na Halmashauri.

Upangaji wa sokoni

7. Mtu ye yote hatatambulika kama mpangaji halali katika eneo la soko la Halmashauri ikiwa hatakuwa na Mkataba wa maandishi na Halmashauri.

Usafi kwenye Soko

8.-(1) Mtu yeyote anayefanya shughuli yoyote katika soko au gulio atawajibika kuzingatia taratibu za usafi zilizowekwa na Halmashauri Na Sheria zingine za nchi.

(2) Mtu ye yote aliyepanga katika soko atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa eneo alilopanga linakuwa safi kwa kuzingatia masharti yafuatayo:-

(a) atunze kizimba chake na vifaa vilivyomo katika hali nzuri na ya usafi kulingana na Sheria na Kanuni za afya.
(b) kuondoa takataka zote na zile zilizofagiliwa katika kizimba na kuzipeleka sehemu ya takataka iliyotengwa na Halmashauri.
(c) kumwaga maji taka kutoka katika kizimba kwa njia ya mifereji au njia nyingine nyingine iliyotengwa kwa ajili hiyo.
(d) nyama, samaki, kuku na utumbo kuwekwa katika chombo kizuri au chombo kitakachotolewa na mwenye

kizimba kwa ajili ya shughuli hiyo.

(e) kutumia vipimo vya uzito na vipimo vinavyokubalika kisheria

Marufuku

9. Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuosha au kusafisha mboga, nyama, samaki au mazao mengine yoyote, chombo au kitu chochote katika eneo la soko au eneo la wazi katika soko isipokuwa sehemu zilizotengwa kwa ajili ya kazi hiyo.

Usimamizi wa magari

10.-(1)Magari yote yanayotumika kusafirisha mazao au bidhaa kwa ajili ya soko lazima yapakuliwe katika eneo au sehemu zilizotayarishwa kwa ajili hiyo.

(2) Dereva atatakiwa kuondoa gari kutoka sehemu iliyotengwa endapo atatakiwa kufanya hivyo na Mkuu wa Soko.

(3) Mkuu wa Soko atakuwa na mamlaka ya kupanga na kusimamia magari yanayoingia na kutoka sehemu zilizopangwa kwa ajili ya magari hayo ili kuzuia msongamano wa magari.

Minada

11. Mazao yatakayoletwa katika Soko kwa ajili ya kuuzwa kwa mnada yatapelekwa kwa Mnadi atakayekuwa ameteuliwa na Kamati ya Soko na kukubaliana na wafanyabiashara kwa ajili hiyo na kila mnadi atayatoa kwa mauzo eneo la mnada lililokubalika au sehemu nyingine kadri Halmashauri itakavyoelekeza.

Kamati za Soko

12.-(1) Kutakuwa na Kamati ya Soko katika kila soko linalomilikiwa na Halmashauri ambayo;

(a) itasajiliwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(b) itachaguliwa na wafanyabiashara wenyewe kwa mujibu wa katiba yao itakayopitishwa na Halmashauri.

(2) Halmashauri inaweza kuvunja Kamati ya Soko ambayo itashindwa kuendesha shughuli yake kwa mujibu wa katiba ya wafanyabiashara wa Soko husika.

Usimamizi wa Masoko

13. Katika usimamzi wa Masoko na ushiriki wake Halmashauri itakuwa mmiliki na msimamizi wa Masoko yote

ambapo :-

(a) itasimamia na kuendeleza masoko yote kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(b) itasimamia usafi na usalama wa masoko.

(c) itasimamia ufikishaji wa huduma za umeme na maji katika masoko.

(d) uendeshaji wa shughuli zake za kila siku za soko utakuwa chini ya Mkuu wa Soko na kamati ya Soko.

(e) itaisaidia Halmashauri kuhakikisha kuwa soko linaendeshwa kwa ufanisi.

Kuteua Wakala

14.–(1) Halmashauri inaweza kumteua wakala ambaye atawajibika katika uendeshaji wa soko kwa niaba ya Halmashauri.

(2) Wakala atakayeteuliwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi atakuwa na madaraka yote ya kiuendeshaji kwa kipindi chote cha mkataba wake wa uwakala.

(3) Wakala atalipwa kulingana makubaliano na Halmashauri.

Kazi za Wakala

15. Wakala atakayeteuliwa kuendesha soko atakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) kukusanya Ada na Ushuru mbalimbali kama atakavyoelelekezwa kwenye Mkataba wake..
(b) kusimamia na kuimarisha upatikanaji wa huduma za ulinzi, maji na umeme katika soko.
(c) kusimamia na kupitia usajili wa wadau wa soko kwa kushirikiana na Kamati ya soko.
(d) kushughulikia usafi na uondoshaji wa taka katika soko.
(e) kutekeleza majukumu mengine yoyote atakayoelekezwa na Halmashauri.

Kamati ya Wadau wa soko

16.-(1) Kutakuwa na Kamati ya Wadau wa soko ambayo itaundwa na Wadau kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Wajumbe wa Kamati ya Wadau wa soko watatokana na kuteuliwa mjumbe mmoja kutoka miongoni mwa wadau wawakilishi wa maeneo ya kibiashara sokoni kutoka kwenye kila kikundi cha Ushirika ndani ya soko.

Vikao vya Kamati ya wadau wa soko

17. Kutakuwa na kikao cha Kamati ya wadau wa soko ambao watakutana mara moja siku ya Alhamisi ya mwisho ya kila mwezi.

Kazi za Kamati ya Wadau wa soko

18. Kazi za Kamati ya Wadau wa soko zitakuwa kama ifuatavyo;

(a) kuhakiki biashara na utendaji wa soko.
(b) kuboresha ustawi wa wanachama wa soko.
(c) kuratibu uendeshaji wa huduma za soko.
(d) kusimamia usafi katika maeneo ya kibiashara sokoni.
(e) kuhakikisha kuwepo nidhamu katika shughuli za soko.

Kuundwa Kamati ndogo

19. Kamati ya Wadau wa soko itaunda Kamati ndogo zifuatazo zenye wajumbe wanne (4) kutoka miongoni mwa wajumbe wa Kamati hiyo:

(a) Kamati ndogo ya Miundombinu na usafi.
(b) Kamati ndogo ya Biashara na Utawala.
(c) Kamati ndogo ya Ulinzi na Usalama

Usajili wa Wadau wa soko

20.-(1) Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi wadau wote wa soko watasajiliwa na Mkuu wa soko kwa kushirikiana na Kamati ya soko.

(2) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote asiye sajiliwa kufanya bishara ndani ya soko.

Kibali cha watumiaji wengine.

21.-(1) Halmashauri kupitia Mkuu wa Soko akishirikiana na Kamati ya Soko itatoa kibali cha kufanya biashara ambayo haikuwepo ndani ya eneo la soko baada ya mwombaji kujaziwa fomu iliyoambatanishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Kibali kilichotolewa katika kifungu cha (1) hapo juu kitadumu kwa muda wa mwaka mmoja na kinaweza kuombwa tena.

Kufuta kibali

22. Mkuu wa Masoko atakifuta kibali kilicho tolewa chini ya Sheria Ndogo hizi endapo mwenye kibali hicho :-

(a) atakuwa na malimbikizo ya madeni ya kodi au ushuru
(b) atakuwa amesimamisha shughuli zake kwa muda wa mwezi mmoja bila ya taarifa.
(c) atakiuka matakwa ya Sheria Ndogo hizi.

Udhibiti wa nidhamu sokoni

23. Ni marufuku kwa mtu ye yote:-

(a) kubandika au kubandua tangazo lolote bila ya idhini ya Mkuu wa Soko.
(b) kuweka bendera za Vyama vya Siasa ndani ya eneo la soko.
(c) kuharibu miundombinu ya soko.
(d) kutumia lugha ya matusi ndani ya soko.

Marufuku

24. Itakuwa ni marufuku chini ya Sheria Ndogo hizi kwa mtu ye yote

(a) kutupa taka hovyo kwenye eneo la soko.
(b) kuingiza vifungashio vya majani ndani ya soko.
(c) kupangisha eneo la biashara kwa mtu mwingine bila kibali cha Halmashauri.

Ada ya kupangisha eneo,vizimba /meza

25.-(1) Kutakuwa na ada ya kupangisha meza eneo la biashara ambayo italipwa na mdau ye yote wa eneo la biashara ndani ya soko, kama inavyoonesha kwenye Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi.

(2) Viwango vya ada vitabadilika kwa kuzingatia bei ya soko thamani na ukubwa wa meza husika kwa wakati huo.

Maeneo ya wazi au barabara

26. Halmashauri itatenga na kuruhusu maeneo ya wazi au barabara kutumika kwa muda maalum kama gulio

Huduma ya maji na umeme

27. Kila Mfanyabiashara atawajibika kugharamia huduma ya ulinzi, usafi, maji na umeme.

Ushuru maegesho

28. Kutakuwa na ushuru utakaolipwa kwa magari yote yatakayoingia ndani ya eneo la soko au barabara za soko kwa ajili ya kupakua au kupakia bidhaa sehemu hiyo kwa viwango vinavyoonekana kwenye Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hizi.

Kupika au kutumia moto ndani ya soko

29. Mtu ye yote hataruhusiwa kupika chakula au kutumia moto kwa njia ye yote ile bila kupata kibali cha maandishi kutoka kwa Mkuu wa Soko.

Makosa

30.-(1) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi iwapo;

(a) atafanya biashara yoyote isiyoruhusiwa na Halmashauri,
(b) atauza pombe ya aina yoyote ndani ya soko bila kibali na leseni ya vileo iliyotelewa na kuidhinishwa na Halmashauri,
(c) ataingiza mifugo sehemu yoyote ndani ya soko isipokuwa iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya biashara ya mifugo,
(d) ataingiza au ataruhusu kuingia mbwa sokoni,
(e) atafanya biashara ya kutembeza bidhaa ndani ya soko bila kibali cha Halmashauri,
(f) atapanga bidhaa chini au kwenye meza na kufanya biashara eneo lolote nje ya soko au katika maeneo yanayozunguka soko.

Adhabu

31. Mtu ye yote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa kiasi cha fedha kisichopungua shilingi laki mbili (200,000/= na kisichozidi shilingi milioni moja (1,000,000/=) au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili (12) na kisichozidi miaka miwili (2) au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

32. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote kiasi cha fedha kisichopungua shilingi laki mbili (200,000/=) na kisichozidi shillingi laki tano (500,000/=) iwapo mkosaji atakiri kwa maandishi kutenda kosa hilo kwa kujaza fomu maalum iliyopo kwenye Jedwali la Nne la Sheria Ndogo hizi na kukubali kulipa ushuru anaodaiwa pamoja na faini.

Tangazo la Serikali namba 47 la Mwaka 2015

33. Sheria Ndogo hizi zinafuta Sheria Ndogo za (Ushuru wa Masoko na Magulio) za Halmashauri ya Jiji la Tanga za Mwaka 2015.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetungwa chini ya kifungu cha 21(1)*

KIBALI CHA KUTUMIA SOKO

1. Jina la mwombaji na anuani yake ………………………………………………..……………………

2. Kibali cha ………………………………………………………………………..……………………….
……………...…………………………………………………………………….…………………………

3. Eneo ambalo kibali hicho kitatumika ………………………………………...…………………….
……………………….........................................................................................................................

4. Muda wa kibali ni kuanzia tarehe …………………………………….… hadi tarehe …………..

5. Masharti ya kutumia kibali hicho

(a) …………………………………….

(b) …………………………………….

(c) ……………………………………..

(d) ……………………………………..

(e)………………………………………

6. Tarehe ya kikao iliyoidhinisha kibali ……..........................................................…………………….
Muhtasari No. …….................................................................................................................. ……

1. Imesainiwa na:

| | |
|---|---|
| Jina ……………………………………… | Na. ………………………………… |
| ……………………………………<br>Mkuu wa Soko | ………………………………….<br>Sahihi ya mwombaji |
| Tarehe ……………………………….. | Tarehe ………………………….. |

Mhuri …………………………………

JEDWALI LA PILI

*(Limetungwa chini ya Kifungu cha 25(1)*

*SEHEMU YA KWANZA*

Ushuru wa kizimba/meza kwenye masoko ya Ngamiani, Mkwakwani, Mgandini na Makorora

| NA | AINA YA MAZAO NA ENEO | KIWANGO CHA KODI KWA SIKU |
|---|---|---|
| 1. | Kizimba | Tshs 1,000/= |
| 2. | Vizimba vya muda | Tshs 1,000/= |
| 3. | Kodi ya duka/kioski<br>Mgandani<br>Mkwakwani<br>Ngamiani<br>Makorora | <br>Tshs 60,000/=<br>Tshs 40,000/=<br>Tshs 80,000/=<br>Tshs 50,000/= |
| 4. | Kodi ya stoo na Ofisi | Tshs 50,000/= |

SEHEMU YA PILI.

Ushuru wa Vizimba kwenye masoko ya Majani Mapana, Mlango wa chuma, Kisosora na Majengo au soko jingine litakaloanzishwa.

| NA. | AINA YA MAZAO NA ENEO | KIWANGO CHA KODI KWA MWEZI |
|---|---|---|
| 1. | Vizimba cha matunda na mbogamboga | Tshs 30,000/= |
| 2. | Vizimba cha magunia | Tshs 30,000/= |
| 3. | Vizimba cha samaki | Tshs 30,000/= |
| 4. | Vizimba cha chai na chakula | Tshs 30,000/= |
| 5. | Vizimba cha nafaka | Tshs 30,000/= |
| 6. | Vizimba cha kuku | Tshs 30,000/= |
| 7. | Vizimba kinginecho | Tshs 30,000/= |
| 8. | Vizimba vya muda | Tshs. 1,000/= kwa siku |
| 9. | Kodi ya Duka/kioski<br>- Kisosora<br>- Mlango wa chuma | <br>Tshs. 20,000/=<br>Tshs.40,000/= |
| 10. | Kodi ya stoo na Ofisi<br>- Mlango wa chuma | <br>Tshs. 60,000/= |
| 11. | Kodi ya kizimba cha Mashine | Tshs.100,000/= |

JEDWALI LA TATU

*(chini ya kifungu cha 28)*

Ushuru wa Magari ya Mizigo

| NA. | | AINA ZA MAZAO | KIWANGO CHA USHURU |
|---|---|---|---|
| | A. | USHURU WA GUNIA | |
| 1. | | DAGAA | 500@ gunia/roba |
| 2. | | VITUNGUU | 500@ gunia/roba |
| 3. | | VIAZI MBATATA | 500@ gunia/roba |
| 4. | | KARANGA | 500@ gunia/roba |
| 5. | | NAZI | 500@ gunia/roba |
| | B. | USHURU WA MATENGA/BOKSI | |
| 6. | | MAEMBE | 500/=@ tenga/boksi |
| 7. | | PAPAI | 500/=@tenga/boksi |
| 8. | | NYANYA | 500/=@ tenga/boksi |
| 9. | | NDIZI | 500/=@ tenga/boksi/Mkungu |
| 10. | | SAMAKI WAKAVU | 500/=@ tenga/boksi |
| 11. | | MABUNGO | 500/=@ tenga/boksi |
| 12. | | SAMAKI WABICHI | 500/=@ tenga/boksi |
| | C. | USHURU WA VIROBA | |
| 13. | | NYANYA CHUNGU | 500/=@ kiroba |
| 14. | | PILIPILI | 500/=@ kiroba |
| 15. | | KAROTI | 500/=@ kiroba |
| 16. | | MATANGO | 500/=@ kiroba |
| 17. | | NDIMU | 500/=@ kiroba |
| 18. | | LIMAU | 500/=@ kiroba |
| 19. | | PESHENI | 500/=@ kiroba |
| 20. | | PARACHICHI | 500/=@ kiroba |
| 21, | | PEASI | 500/=@ kiroba |
| 22. | | EMBE | 500/=@ gunia/roba |
| 23. | | MACHUNGWA | 500/=@ gunia/roba |

| NA. | | AINA ZA MAZAO | KIWANGO CHA USHURU |
|---|---|---|---|
| 24. | | VIAZI VITAMU | 500/=@ gunia/roba |
| 25. | | MIHOGO | 500/=@ gunia/roba |
| 26. | | KUNDE | 500/=@ gunia/roba |
| 27. | | NJEGERE | 500/=@ gunia/roba |
| 28. | | CHOROKO, MBATATA, MAGIMBI | 500/=@ gunia/roba |
| 29. | | Endapo hajalipia kwenye geti inayodhibiti ushuru wa mazao, atatozwa 5% ya bei ya mazao. | |
| 30. | | Ushuru wa bidhaa zisizo katika magunia/kiroba/tenga/box Tsh. 10,000 kwa tani moja | |

JEDWALI LA NNE
HATI YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

(*Chini ya Kifungu cha 33)*

Mimi …………………………………………… (*jina la mtenda kosa*) ambaye ninaishi ……………………..(*mahali*) na kazi yangu ni………………………………, ninatambua na kukiri kuwa nimefanya kosa ………………………………………………. (*Aina ya kosa*) ikiwa ni kinyume na kifungu cha………………… cha Sheria Ndogo za (Ushuru wa masoko,minada na magulio) za Halmashauri ya Jiji la Tanga za Mwaka 2019.

Kwahiyo, kwa hiari yangu mwenyewe pasipo kushawishiwa na mtu yeyote nakubali kulipa faini iliyoainishwa kwenye Sheria Ndogo hizi iwapo Mkurugenzi atatekeleza madaraka aliyopewa chini ya kifungu cha 33 cha Sheria Ndogo hizi.

Saini: ……………………….......................

Mbele yangu:-
Jina: ……………………………………….
Saini: ……………………………………….
Wadhifa: …………………………………….

Lakiri ya Halmashauri ya Jiji la Tanga imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa katika kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Jiji la Tanga kilichofanyika Tarehe 30 mwezi Januari mwaka 2019 na kushuhudiwa Lakiri hiyo ikibandikwa mbele ya:-

**L.S**

…………………………………………………………

DAUDI R. MAYEJI,
*Mkurugenzi wa Jiji*
*Halmashauri ya Jiji la Tanga*

…………………………………………………………

SELEBOSS M. MUSTAFA,
*Mstahiki Meya*
*Halmashauri ya Jiji la Tanga*

NAKUBALI,

DODOMA,
1Januari, 2019

SELEMANI S. JAFO (MB.),
*Waziri wa Nchi ofisi ya Rais TAMISEMI*